**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA**

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**[***Imetolewa chini ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023***]**

**08 Mei, 2025**

## YALIYOMO

*Ukurasa*

**YALIYOMO** ........ **i**
**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ **ii**
**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ **iii**
**SEHEMU YA KWANZA** ........ **1**
**1.0 UTANGULIZI** ........ **1**
**1.1 Maelezo ya Awali** ........ **1**
**1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati** ........ **2**
**1.3 Mawanda (Scope) ya Uchambuzi** ........ **3**
**SEHEMU YA PILI** ........ **4**
**2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI** ........ **4**
2.1 Maelezo ya Jumla ........ 4
2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 ........ 5
2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ........ 5
2.2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ........ 7
2.2.3 Makusanyo ya Maduhuli ........ 13
2.2.4 Hali ya upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida ........ 15
2.2.5 Hali ya upatikanaji wa fedha za Maendeleo ........ 17
2.2.6 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 ........ 20
**SEHEMU YA TATU** ........ **24**
**3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ........ **24**
3.1 Uchambuzi wa Malengo na Vipaumbele ........ 24
3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ........ 25
3.2.1 Makadirio ya Maduhuli yatakayokusanywa ........ 25
3.2.2 Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ........ 28
3.2.3 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ........ 29
3.2.4 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti ya Serikali ........ 31
**3.3 MAONI NA USHAURI WA KAMATI** ........ **33**
3.3.1Maoni ya Kamati ........ 33
3.3.2Ushauri wa Kamati ........ 37
3.3.3Hitimisho ........ 41

## ORODHA YA VIFUPISHO

1. **CCM** - Chama cha Mapinduzi
2. **OC** - Other Charges
3. **PE** - Personal Emolument
4. **RUWASA** - Rural Water Supply and Sanitation Agency
5. **SDGs** - Sustainable Development Goals
6. **TAMISEMI** - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
7. **TANGA - UWASA** - Tanga Urban Water Supply and Sanitation Authority

# ORODHA YA MAJEDWALI

**JEDWALI NA. 1:** Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........ 14

**JEDWALI NA. 2:** Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa na kupokelewa hadi Februari, 2025 ........ **16**

**JEDWALI NA. 3:** Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo hadi Februari, 2025 ........ 18

**JEDWALI NA. 4:** Ulinganisho wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026........ 26

**JEDWALI NA. 5:** Mchanganuo wa Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026 ........ 28

J**EDWALI NA. 6:** Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo Fungu 49 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2024 na 2025/2026 ........ 30

**JEDWALI NA. 7:** Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali 2025/2026........ **32**

**JEDWALI NA. 8:** Orodha ya Taasisi za Serikali zinazodaiwa na Mamlaka za Maji . 35

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Mkutano huu wa kumi na Tisa ambao ni wa mwisho katika Bunge hili la Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari,

2023, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu Kuu tatu kama ifuatavyo: -

(a) Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(b) Sehemu ya Pili inabainisha Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2024/2025; na

(c) Sehemu ya Tatu inabainisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2025/2026

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6(6) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira. Kwa madhumuni ya taarifa hii, Wizara ya Maji **(Fungu 49)** inahusika**.**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeweka masharti yanayoitaka Kamati kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Aidha, Masharti ya Kanuni ya 118 (4) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge

Toleo la Februari, 2023 yanazitaka Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Maji na Mazingira kuchambua Taarifa za Bajeti kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 25- 26 Machi, 2025, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maji **Fungu 49** kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## 1.3 Mawanda (Scope) ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji ina Fungu Moja **(Fungu 49).**

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inafafanua Uchambuzi katika maeneo yafuatayo: **-**

(a) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na;

(b) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ikilinganishwa na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Njia iliyotumika kufanya uchambuzi inajumuisha kulinganisha hali ilivyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Njia ya ukokotoaji wa asilimia imetumika kubaini hatua inayofikiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha na kujiridhisha na uwezekano wa mipango inayolengwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa kutumia uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilijikita katika maeneo Makuu Matano yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Matokeo ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Hali ya Makusanyo ya Maduhuli

(iv) Hali ya Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 na;

(v) Utekelezaji wa mipango iliyowekwa kwa Mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, kwa urahisi wa ufuatiliaji na uamuzi wa kibunge, naomba kubainisha matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitoa Ushauri katika maeneo Kumi na Nne (14). Naomba kulijulisha Bunge lako

Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Ushauri wa Kamati umezingatiwa.

(a) Mfano wa Ushauri uliozingatiwa unahusu Serikali, kwa kutumia taarifa ya utabiri wa hali ya hewa, kuandaa mkakati mahsusi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuchimba mabwawa/visima na kupanda miti rafiki kwa mazingiza ili kulinda vyanzo vya maji. **Utekelezaji ulioripotiwa unaonesha kuwa** Wizara iliandaa Mkakati wa kujenga Mabwawa mwaka 2022/2023 hadi 2025/2026. Vile vile Wizara iliandaa na inaendelea kutekeleza Mipango ya uhifadhi wa vidakio vya maji nchini kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi mwaka 2035. Kwa mwaka 2024/2025 shughuli zilizotekelezwa kupitia mipango hiyo ni:-

 (i) Upandaji wa miti rafiki kwa mazingira **95,838** katika maeneo ya vyanzo vya maji ili kuimarisha ustahimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi kwa jamii.

 (ii) Wizara inaendelea na mradi wa uchimbaji wa visima vitano (5) kwa kila Jimbo la uchaguzi ili kuyapatia huduma ya maji maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma. Hadi mwezi Februari, 2025 jumla ya visima **657** vimechimbwa na kuanza kutoa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kutekeleza ushauri wa Kamati. Ni rai ya Kamati kwamba Serikali iendelee kutekeleza kikamilifu na kwa haraka maeneo ambayo utekelezaji wake umefanyika kwa kiwango cha chini. Mfano wa Ushauri huo ni **Serikali kulipa malimbikizo ya madeni yote ya Wakandarasi.** Utekelezaji ulioripotiwa unaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 hadi kufikia mwezi Februari 2025 Serikali imelipa Wakandarasi, Wataalam Washauri na Wazabuni jumla ya **Shilingi 358,509,163,062.72 kati ya Shilingi 893,234,234,587.03 na hivyo** Wizara ya Maji kuendelea kudaiwa na Watoa huduma kiasi cha **Shilingi 534,725,071,524.31.**

**Mheshimiwa Spika,** mara zote ushauri unaotolewa Bungeni unalenga kuboresha shughuli za umma kwa maslahi ya taifa. Hivyo, kuzingatiwa kwa ushauri huo kunatimiza azma ya kuboresha ustawi wa Wananchi.

### 2.2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia Masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kwa kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii katika Mikoa ya Tabora, Kigoma, na Katavi. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu matokeo ya Ukaguzi wa Miradi hiyo kama ifuatavyo: -

**(a) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Maji katika Kijiji cha Kizengi, Wilaya ya Uyui**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Uyui Mkoani Tabora kwa gharama ya **Shilingi 4,128,487,640.02** ambapo chanzo Kikuu cha fedha hizo ni Mfuko wa Taifa wa Maji. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, mradi ulitengewa kiasi cha **Shilingi 3,828,487,640.00.** Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Machi, 2025 mradi huu umepokea kiasi cha **Shilingi 1,300,000,000** sawa na **asilimia 34** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kazi zilizotekelezwa katika Mradi huu ni pamoja na maandalizi ya mradi, uchimbaji wa Msingi na ujenzi wa tuta kuu, uimarishaji wa tuta kuu na ujenzi wa *intake tower* na *outlet chamber.* Aidha, kazi zilizobaki ili kukamilisha mradi huu zinahusisha uchimbaji wa utoro wa maji wenye **urefu wa Mita 950,** kukamilisha ujenzi wa tuta kwa kimo cha **Mita 0.44**, ujenzi wa tuta elekezi na miundombinu ya utoro wa maji.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 60** na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2025 ambapo utanufaisha Wananchi wa Vijiji 13 ambavyo ni Kizengi, Kabisile, Gengesita, Miyenze, Mwamdaki, Malongwe, Mpumbuli, Loya, Lutona, Mwamabondo, Migongwa, Mwamdalaigwe na Miswaki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi huu ingawa fedha zilizopokelewa ni asilimia **34** tu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji huo umechangiwa na matumizi ya Seti za Mitambo ya Kuchimba Mabwawa iliyonunuliwa na Serikali na hivyo matumizi hayo kupunguza kwa kiasi kikubwa gharama za utekelezaji wa Mradi.

**b) Mradi wa Maji wa Munanila – Nyakimue**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Buhigwe Mkoa wa Kigoma**.** Mradi unatekelezwa kwa fedha kutoka vyanzo viwili ambavyo ni Serikali kupitia RUWASA na fedha za Miradi ya nyongeza kutoka benki ya maendeleo ya Afrika kupitia mradi wa barabara ya Kasulu – Manyovu. Mradi huu unatekelezwa kwa Mkataba wa **Shilingi 9,765,183,456** ambapo hadi mwezi Machi, 2025, Mkandarasi amelipwa **Shilingi 5,020,660,985.23.** Aidha, baada ya kukamilika kwake mradi huu unatarajiwa kunufaisha wakazi wapatao **66,406** katika Vijiji 8 ambavyo ni Munanila, Nyakimue, Mkatanga, Musagara, Kitambuka, Kibwigwa, Bweranka na Kibande.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/25 kiasi cha **Shilingi 1,162,147,707.95** kiliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Hadi kufikia

mwezi Machi, 2025 mradi umepokea kiasi cha **Shilingi 1,137,054,574.66** ambayo ni sawa na **asilimia 97.8** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, utekelezaji wa Mradi umefikia **asilimia 67** ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na ununuzi wa bomba zenye urefu wa **Mita 87,866.62**, ujenzi wa nyumba za mitambo, ujenzi wa matenki mawili yenye ujazo wa **Lita 1,000,000,000** na ujenzi wa vituo vinne vya kuchotea maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Ni rai ya Kamati kwamba, Serikali itaendelea kutenga fedha na kuzitoa inavyostahili ili kufanikisha utekelezaji madhubuti wa mradi huo.

**c) Mradi wa ujenzi wa Bwawa la kutibu Majitaka katika Manispaa ya Mpanda, Mkoani Katavi**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 1,197,060,573.47** na ulianza kutekelezwa tarehe 14 Juni, 2024 ambapo unatarajiwa kukamilika tarehe 13 Disemba, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/25 mradi ulitengewa kiasi cha **Shilingi 267,857,142.00.** Hadi kufikia Machi, 2025 Mkandarasi amelipwa jumla ya **Shilingi 152,000,000.**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2025 utekelezaji wa Mradi umefikia **asilimia 35** ambapo kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(a) Uchongaji wa barabara kuelekea eneo la mradi;
(b) Usafishaji wa eneo la ujenzi;
(c) Umwagaji wa zege katika msingi wa Mabwawa; na
(d) Ujenzi wa nyumba ya mlinzi.

Aidha, kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na -

(a) Ujenzi wa fensi yenye urefu wa **Mita 148.3** na upana wa **Mita 86;**
(b) Ujenzi wa miundombinu ya kukaushia tope litakalozalishwa; na
(c) Ujenzi wa Kuta za Mabwawa.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatarajiwa kunufaisha Wananchi wapatao **245,764,** kuimarisha uwezo wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda, kuboresha afya ya Jamii na kuwezesha upatikaji wa maji kwa shughuli mbalimbali ikiwemo Kilimo.

**d) Mradi wa ujenzi wa Kuboresha Miundombinu ya Uzalishaji na Usambazaji Maji Kanoge katika Manispaa ya Mpanda**

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa maji wa Kanoge umeandaliwa na Wizara ya Maji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa lengo la kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo pampu zinazotumia Mfumo wa jua na ujenzi wa Vituo vya Maji ili kuhakikisha Jamii zinazozunguka maeneo ya vyanzo vya maji zinanufaika na miradi hiyo. Mradi huu unagharimu kiasi cha **Shilingi 2,082,116,023.**

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ulianza mwanzoni mwa mwezi Machi 2025 kwa kumkabidhi Mkandarasi na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2025. Hadi mwezi Machi, 2025, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 10.** Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na :-

(a) Uchimbaji wa Mtaro kwa **Kilomita 6.5** kati ya **Kilomita 19.5** zinazotarajiwa kuchimbwa;

(b) Ulazaji wa Mabomba urefu wa **Kilomita 3.5**; na

(c) Urejeshaji wa huduma ya Maji kwa Wananchi wa Kanoge.

**Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa mradi huu kunatarajiwa kuongeza miundombinu ya uhifadhi maji kutoka **Lita 3,730,000** hadi kufikia **Lita 4,730,000** na kuongeza uzalishaji wa maji **Lita 2,000,000** kwa siku

na kufikiwa kiwango cha **Lita 8,266,500** kwa siku katika Manispaa ya Mpanda. Aidha, wakazi wapatao **43,962** wanatarajiwa kunufanikisha na mradi**.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuendelea na utekelezaji wa Miradi kwa kuzingatia mahitaji ya Wananchi waliopo kando na vyanzo vya maji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Miradi ya Maji iliyotembelewa na kukaguliwa. Hata hivyo, inasisitiza kuwa fedha zinazotengwa zitolewe kwa wakati ili kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

### 2.2.3 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maji (**Fungu 49**) iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,400,001,000**. Hadi mwezi Februari, 2025, makusanyo halisi yalikuwa **Shilingi 782,222,941.00** sawa na **asilimia 55.9** ya lengo la mwaka. **Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli umeainishwa kwenye Jedwali Na. 1**

**JEDWALI NA. 1: Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2024/2025 | MAKUSANYO HADI FEBRUARI,2025 | ASILIMIA YA LENGO |
|---|---|---|---|
| Mauzo ya Nyaraka za Zabuni | 1,000.00 | 3,900,000.00 | |
| Malipo kwa ajili ya leseni kwa Makampuni ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji | 300,000,000.00 | 217,820,550.00 | 72.6 |
| Ada kwa huduma za Maabara | 1,100,000,000 | 560,502,391.00 | 51 |
| **JUMLA** | **1,400,001,000** | **782,222,941.00** | **55.9** |

**Chanzo:** Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa: -

**(a)** Mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Wizara ya Maji kwa kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji wa Bajeti ni **asilimia 55.9** ya lengo la ukusanyaji kwa mwaka. Ukusanyaji huu uko chini ya kiwango kilichotarajiwa kwa kipindi hiki ambacho kilipaswa kuwa zaidi ya **asilimia 66.6.** Hali hii inahitaji msukumo mkubwa wa Serikali ili lengo la Makusanyo ya Maduhuli lifikiwe ifikapo Juni 2025;

**(b)** Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli kutokana na Leseni za Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji ulifikia **asilimia 72.6**. Kiwango hiki cha Makusanyo ni dalili nzuri kwamba Wizara itaweza kufikia lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kutokana na chanzo hicho ifikapo mwezi Juni, 2025. Vile vile hali hiyo, inaonesha kwamba, upangaji wa lengo ulizingatia uhalisia;

**(c)** Mwenendo wa ukusanyaji wa Ada kwa Wateja wanaopata huduma za Maabara za ubora wa maji ulifikia **asilimia 51.** Hali hii inatia shaka iwapo Wizara itaweza kufikia lengo la makusanyo ifikapo mwezi Juni, 2025**.** Hata hivyo, mwenendo huu unaashiria kuwa iwapo huduma za Maabara zitaboreshwa na kusimamiwa ipasavyo, makusanyo ya Maduhuli yanaweza kuongezeka, hivyo kufikia lengo lililokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, uwekezaji wa kutosha katika Leseni za Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji utachangia kuongeza Mapato ya Serikali, na hivyo kuleta tija iliyokusudiwa kwa Wananchi.

### 2.2.4 Hali ya upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha ni hatua muhimu katika utekelezaji wa Bajeti. Aidha, mwenendo wa kiwango cha fedha kinachopatikana kwa mwaka mmoja ni muhimu katika uamuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa mantiki hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha kwa bajeti ya mwaka 2024/2025 na matokeo ya uchambuzi yameonesha mambo yafuatayo: -

### (a) Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maji iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 69,662,959,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 11.1** ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 17,542,691,840** ni za Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 52,120,267,160** ni za Mishahara ya Wizara na Taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Februari, 2025, fedha zilizotolewa kwa ajili ya OC ni **Shilingi 7,690,721,225.00** sawa na **asilimia 43.8** ya lengo, na kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya Mishahara ni **Shilingi 30,680,936,908.00** sawa na **asilimia 58.9** ya lengo.

**JEDWALI NA. 2: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa na kupokelewa hadi Februari, 2025**

| Fedha iliyoidhinishwa 2024/2025 | | Fedha iliyopokelewa hadi Februari 2025 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA OC** | 17,542,691,840 | 7,690,721,225.00 | 43.8 |
| **FEDHA ZA MISHAHARA** | 52,120,267,160 | 30,680,936,908.00 | 58.9 |
| **JUMLA** | **69,662,959,000.00** | **38,371,658,133.00** | **55** |

**Chanzo:** Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi katika jedwali unaonesha kwamba utolewaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida ambazo zinakusudiwa kutumika katika uendeshaji wa shughuli za uimarishaji wa huduma za Maji Mijini na Vijijini hadi kufikia mwezi Februari 2023, ni **asilimia 55** ya Bajeti

iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo. Upatikanaji huo wa fedha uko chini ukilinganishwa na kiasi kilichopaswa kufikiwa kwa kipindi kama hiki ambao ni **asilimia 66.6. Ni rai ya Kamati kwamba Serikali ihakikishe inatoa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge ifikapo tarehe 30 Juni 2025 ili kukidhi matarajio ya wananchi ya kupata huduma ya majisafi na salama.**

### 2.2.5 Hali ya upatikanaji wa fedha za Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha, 2024/25, **Fungu 49** liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 558,115,379,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 340,463,656,000** ni fedha za ndani kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali na Mfuko wa Taifa wa Maji na **Shilingi 217,651,723,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Februari, 2025, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 396,939,393,090.53** sawa na **asilimia 71.1** ya lengo la fedha za Maendeleo kwa mwaka. Mchanganuo wa upatikanaji wa fedha za Maendeleo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 03**

**JEDWALI NA. 3: Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo hadi Februari, 2025**

| FEDHA ZILIZOIDHINISHWA 2024/2025 | | FEDHA ZILIZOPOKELEWA HADI FEBRUAI, 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 340,463,656,000 | 295,636,971,762.42 | **86.8** |
| **FEDHA ZA NJE** | 217,651,723,000 | 101,302,421,328,.11 | **46.8** |
| **JUMLA** | 558,115,379,000 | 396,939,393,090.53 | **71.1** |

**Chanzo:** Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya Uchambuzi wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha kwa ajili kugharimia Miradi ya Maendeleo inayolenga kuimarisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama ulifikia **asilimia 71.1** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. **Upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa wakati ni kiashiria kwamba Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa itakamilika kama ilivyokusudiwa ifikapo Juni, 2025;**

(b) Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **aslimia 86.8** ya Bajeti iliyoidhidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. **Hali hii inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kumtua mama ndoo kichwani na ni kasi nzuri ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM**

**ambayo inaelekeza Serikali kuhakikisha kuwa huduma ya majisafi na salama inawafikia wananchi wa Vijijini kwa asilimia 85 na Mijini kwa asilimia 95 ifikapo 2025.**

(c) Kwa upande wa fedha kutoka nje upatikanaji wake ulifikia **asilimia 46.8** ya Bajeti iliyoidhinidhwa na Bunge. **Hali hii inaonesha kwamba upo uwezekano mkubwa wa kutofikia lengo ifikapo Juni,2025. Ni rai ya Kamati kwamba Serikali inapopanga bajeti izingatie uhalisia kwani kwa kutopokea kiasi cha kutosha cha fedha za nje ipo miradi itakayokwama. Aidha, ni wakati mwafaka kwa Serikali kuendelea kupunguza utegemezi kutoka nje.**

(d) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia Upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa wakati hususani fedha za ndani. Hali hii inaonyesha dhamira ya kweli ya Serikali katika kuhakikisha kwamba nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na kuimarisha huduma ya Majisafi na Salama. **Ni rai ya Kamati kwamba kiasi cha fedha kilichobaki kitatolewa mapema kabla ya mwezi Juni, 2025 ili Miradi iliyopangwa iweze kukamilika kwa asilimia 100.** Aidha, ni matarajio ya Kamati kuwa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha 2024/2025 utafaa kutumika katika upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ili

miradi itakayokuwa imepangwa kutekelezwa ikamilike kwa wakati.

### 2.2.6 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2024/2025

#### (a) Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Wizara ya Maji

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ililenga kufanikisha utekelezaji wa Mipango na majukumu ya Wizara ya Maji na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Ili kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa Bajeti hiyo, Kamati ilidadisi utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika maeneo Makuu matatu ya Sekta ya Maji. Maeneo hayo ni: -

(i) Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji;

(ii) Huduma ya Majisafi na usafi wa mazingira Vijijini na Mijini;

(iii) Uratibu na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zake;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Mafanikio yaliyopatikana hadi mwezi Februari, 2025, ni pamoja na:-

(i) Kukarabatiwa kwa **Vituo 127** na kujengwa kwa **Vituo 9** vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji nchini;

(ii) Kutambuliwa kwa vyanzo vipya **121** vya maji juu ya ardhi, kuwekwa mipaka kwenye vyanzo vya maji **29** ambapo vigingi (beacon) **4,977** vimesimikwa na

kupanda miti rafiki wa Mazingira **95,838** kwenye vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini;

(iii) Kutatuliwa kwa migogoro yote **19** ya matumizi ya maji iliyoripotiwa;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa Bwawa la Kidunda unaogharimu **Shilingi Bilioni 329.5** ambapo hadi mwezi Februari 2025, ujenzi wa Bwawa hilo umefikia **asilimia 28**;

(v) Skimu **959** za maji Vijijini zilihakikiwa ubora wa maji ambapo skimu **577** sawa na **asilimia 64.1** zilikidhi ubora; skimu **268** za maji Mijini zilihakikiwa ambapo skimu **63** sawa na **asilimia 52.1** zilikidhi ubora. Hata hivyo zipo changamoto zilizobainika katika uchunguzi wa ubora wa maji. Changamoto hizo ni pamoja na viwango vikubwa vya madini ya Chuma, Manganese na Chumvichumvi katika Mikoa ya Mtwara na Lindi; pamoja na kiwango kikubwa cha madini ya Fluoride katika Mikoa ya Arusha, Manyara na Singida, Nitrate Mkoa wa Dodoma na uwepo wa vijidudu vya bakteria katika maji;

(vi) Kukamilika kwa miradi **294** ambapo Wananchi wapatao **2,316,005** wamenufaika na huduma ya maji katika Vijiji **836.**

**Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa miradi hiyo kumechangia kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa

huduma ya maji maeneo ya Vijijini kufikia **asilimia 83** Mwezi Februari 2025.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na utekelezaji huo, Kamati inampongeza kwa dhati Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso (Mb) Waziri wa Maji pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi Mwajuma Waziri kwa usimamizi madhubuti wa kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa zinatumika ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 zipo changamoto za kuchelewa kwa Utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maji. Changamoto hizo ni pamoja na;

a) **Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi mikubwa ya Kimkakati ya maji.**

**Mheshimiwa Spika,** uwekezaji kwenye Miradi ya Maji unahitaji fedha nyingi kwa wakati mmoja, lakini upatikanaji wa fedha umekuwa si kwa kasi iliyokusudiwa. Kwa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, Wizara inakabiliwa na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati inayohusisha uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga Mabwawa na miundombinu ya kutoa maji kwenye vyanzo vya maji vya uhakika kama Maziwa, na Mito kwenda maeneo yenye uhaba wa maji.

**b) Uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji**

**Mheshimiwa Spika,** uelewa mdogo wa Jamii juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na ongezeko la watu linalosababisha kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi ni vyanzo Vikuu vya uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji.

**c) Mabadiliko ya tabianchi**

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi yanaathiri nchi yetu kwa kusababisha mafuriko na ukame wa muda mrefu, hivyo kuchangia kupungua au kukauka kwa vyanzo vya maji, kupungua kwa uzalishaji wa maji na kusababisha kuongezeka kwa mgao wa maji pamoja na kuharibika kwa miundombinu ya maji kutokana na mafuriko;

**d) Uendelevu wa miradi ya maji Vijijini**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi za Serikali katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji Vijijini bado kuna changamoto ya uendelevu wa miradi ya maji katika baadhi ya maeneo. Hali hiyo inachangiwa na kukauka kwa vyanzo vya maji, Wananchi kushindwa kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo kutokana na makusanyo hafifu ya mauzo ya maji, pamoja na uharibifu wa miundombinu ya maji.

**SEHEMU YA TATU**

# 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

## 3.1 Uchambuzi wa Malengo na Vipaumbele

**Mheshimiwa Spika,** usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji ni msingi wa shughuli zote za maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii kwa ajili ya usalama wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Malengo na vipaumbele vilivyoainishwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, vinaendana na majukumu ya Msingi ya Wizara ya Maji, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 inayobainisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wote; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025; inayoelekeza Serikali kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa Wananchi waishio Vijijini unafikia zaidi ya **asilimia 85** na zaidi ya **asilimia 95** kwa Mijini; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano Awamu ya tatu 2021/2022- 2025/2026; Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2016-2030) na ahadi mbalimbali za Viongozi wa Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Sekta ya Maji inafikia malengo yaliyobainishwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza maeneo ya Vipaumbele yafuatayo: -

(a) Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji;
(b) Usimamizi wa huduma za ubora wa maji;
(c) Huduma ya majisafi na usafi wa mazingira Vijijini;
(d) Huduma ya majisafi na usafi wa mazingira Mijini;
(e) Kupunguza upotevu wa Maji na;
(f) Kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zake.

## 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2025/2026

### 3.2.1 Makadirio ya Maduhuli yatakayokusanywa

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ya Maji (**Fungu 49)** inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 1,700,001,000,** kutokana na vyanzo vya Leseni kwa Kampuni za Utafiti na uchimbaji wa Visima vya maji, Tozo mbalimbali kwa wateja wanaopata huduma ya Maabara za ubora wa maji na vibali vya matumizi ya maji katika Mabonde. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,400,001,000/=** ni ada za huduma za Maabara za maji na **Shilingi 300,000,000/=** zinatokana na Leseni kwa Kampuni za Utafiti na uchimbaji wa Visima vya maji, na vibali vya matumizi ya maji katika Mabonde.

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilifanya ulinganisho wa Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Maduhuli yanayokadiriwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi wa ulinganisho huo unaonekana katika **Jedwali Na. 04**.

**JEDWALI NA. 4: Ulinganisho wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MADUHULI 2024/2025 | MAKADIRIO YA MADUHULI 2025/2026 | % ONGEZEKO/PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| **Mauzo ya Nyaraka za Zabuni** | 1,000.00 | 1,000.00 | **-** |
| **Leseni za Kampuni za Utafiti** | 300,000,000.00 | 300,000,000.00 | **-** |
| **Ada - Huduma za Maabara** | 1,100,000,000.00 | 1,400,001,000.00 | **21.4** |
| **JUMLA** | **1,400,001,000.00** | **1,700,001,000.00** | **17.6** |

**Chanzo: Randama ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya Uchambuzi yanaonesha kuwa: -

(i) Lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 limeongezeka, kwa **asilimia 17.6** ikilinganishwa na Makadirio ya Makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa upande wa Leseni za Kampuni za utafiti halijaongezeka. Uchambuzi huo unaonesha kuwa upangaji wa makadirio umezingatia hali halisi ya utekelezaji wa mwaka wa fedha unaoisha.

(iii) Makadirio ya makusanyo ya Maduhuli kutokana na Ada za huduma za maabara za maji umeongezeka kwa **asilimia 21.4.** Uchambuzi unaonesha kuwa Serikali haijazingatia uhalisia katika kupanga ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo makusanyo yalikuwa **asilimia 51** hadi mwezi Februari,2025.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hilo. Hata hivyo ni rai ya Kamati kwamba Serikali iweke Mkakati mahsusi wa kuwezesha kukusanya kiasi kilichopangwa wakati wa utekelezaji ili kufikia malengo yaliyowekwa. Hii ni kutokana na uzoefu wa makusanyo yaliyopatikana kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2024/2025 kuwa chini ya kiwango.

### 3.2.2 Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2025/2026,

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Maji (**Fungu 49)** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 73,779,579,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 18,081,382,000** sawa na **asilimia 25.0** ni kwa ajili ya kugharimia Matumizi Mengineyo (OC), na **Shilingi 55,698,197,000** sawa na **asilimia 75.0** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake. **Jedwali Na. 5** linaonesha mchanganuo wa ulinganisho wa bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka unaoisha na mwaka wa fedha 2025/2026.

**JEDWALI NA. 5: Mchanganuo wa Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026**

| **ULINGANISHO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA FUNGU 49 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| AINA YA MATUMIZI | BAJETI MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO MWAKA 2025/2026 | ONGEZEKO/ PUNGUFU | ASILIMIA YA ONGEZEKO/PUNGUFU |
| Mishahara | 52,120,267,160 | **55,698,197,000** | **3,577,929,840.00** | 6.4 |
| OC | **17,542,691,840** | **18,081,382,000** | **538,690,160.00** | 3 |
| JUMLA | **69,662,959,000.00** | **73,779,579,000.00** | **4,116,620,000.00** | 5.6 |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Maji (**Fungu 49**) kwa mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa: -

(a) Bajeti ya Wizara ya kuimarisha huduma ya majisafi na salama imeongezeka kwa **asilimia 5.6**.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti hiyo ya Matumizi ya Kawaida. Ni rai ya Kamati kuwa Bajeti hii itatolewa kama ilivyopangwa ili shughuli za usimamizi na uendeshaji wa rasilimali za maji zisimamiwe kwa ukamilifu.

### 3.2.3 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Maji inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 943,115,379,000.00** kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 340,463,656,000.00** sawa na **asilimia 36** ni fedha za ndani na **Shilingi 602,651,723,000.00** sawa na **asilimia 64** ni fedha za nje. **Jedwali Na. 6** linaonesha mchanganuo wa ulinganisho wa fedha za Matumizi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na 2025/2026.

**JEDWALI NA. 6: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo Fungu 49 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2024 na 2025/2026**

| ULINGANISHO WA BAJETI YA MATUMIZI YA MAENDELEO FUNGU 49 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **AINA YA BAJETI** | **MAKADIRIO MWAKA 2024/2025** | **MAKADIRIO MWAKA 2025/2026** | **ONGEZEKO/ PUNGUFU** | **ASILIMIA YA ONGEZEKO/ PUNGUFU** |
| **NDANI** | 340,463,656,000.0 | 340,463,656,000.00 | - | **-** |
| **NJE** | 217,651,723,000.00 | 602,651,723,000.00 | 385,000,000,000 | **63.9** |
| **JUMLA** | **558,115,379,000.00** | **943,115,379,000.00** | **385,000,000,000** | **40.8** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Maji (Fungu 49) kwa mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa:

(a) Bajeti ya Wizara ya Maji kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 40.8** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025. Kamati inaipongeza Serikali kwa usikivu na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati kwa kuongeza bajeti ya kugharamia miradi ya maendeleo.

(b) Bajeti ya fedha za nje imeongezeka kwa asilimia **63.9 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025. Hali hii ni dalili nzuri kwamba Nchi yetu ina mahusiano mazuri na washirika wa maendeleo. Hata**

**hivyo ni rai ya Kamati kwamba Serikali ifuatilie kwa karibu ili fedha hizi zitolewe kama zilivyopangwa ili kutokwamisha utekelezaji wa miradi**

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo, Kamati imeridhika kwamba Bajeti hii imezingatia azma ya Serikali iliyotamkwa katika Ibara ya 100, Ukurasa wa 149 wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020-2025. Azma hiyo ni kuona kwamba, nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na kwamba huduma ya majisafi na salama inaendelea kuimarishwa na kuwafikia Wananchi zaidi ya asilimia **85 Vijijini** na **95 kwa Mijini** ifikapo mwaka 2025. Ongezeko hilo la Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 linaakisi lengo hilo. Msistizo wa Kamati kwa Serikali ni kuhakikisha kuwa Bajeti inayoidhinishwa na Bunge inatekelezwa ipasavyo.

### 3.2.4 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti ya Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ili kubaini ongezeko/ pungufu la Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali.

**Mheshmiwa Spika,** jumla ya fedha inayoombwa na Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni **Shilingi**

**1,016,894,958,000.00** huku Bajeti Kuu ya Serikali ikiwa ni **Shilingi 57,040,252,000,000.25,** sawa na **asilimia 1.8** ya bajeti Kuu ya Serikali

**JEDWALI NA. 7: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali 2025/2026**

| **ULINGANISHO WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI DHIDI YA BAJETI KUU YASERIKALI 2025/2026** | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA YA BAJETI** | **BAJETI YA SERIKALI** | **BAJETI YA WIZARA YA MAJI** | **ASILIMIA** |
| **MATUMIZI YA MAENDELEO** | 19,471,000,000,000.41 | 943,115,379,000.00 | **4.8** |
| **JUMLA BAJETI YA MAENDELEO NA MATUMIZI YA KAWAIDA** | 57,040,252,000,000.25 | 1,016,894,958,000.00 | **1.8** |

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Ulinganisho huo unaonesha kuwa: -

(a) Bajeti ya Wizara ya Maji ni **asilimia 1.8** ya Bajeti Kuu ya Serikali. Sawa na ongezeko **la asilimia 0.5** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 ambayo ilikuwa **asilimia 1.3.** Hali hii inaashira kwamba kwa kiasi fulani Bajeti Kuu ya Serikali imezingatia umuhimu wa majukumu ya Wizara ya Maji;

(b) Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji ni **asilimia 4.8** ya Bajeti Kuu ya Serikali ya Maendeleo ambayo ni **asilimia 34.1** ya Bajaeti Kuu ya Serikali.

(c) Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji imeongezeka kwa **asilimia 3.4** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 ambayo ilikuwa **asilimia 1.1** ya bajeti Kuu ya Serikali ya Maendeleo.

(d) **Mheshimiwa Spika**, kwa Uchambuzi huo, Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mtazamo huo wa kimaendeleo katika Sekta ya Maji nchini. Uchambuzi wa Takwimu hizi ni ishara ya hatua za kutimiza ahadi ya Serikali katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020-2025 Ibara ya 100 Ukurasa wa 149 ya kuimarisha huduma ya majisafi na salama kwa Wananchi na kuwafikia wakazi **asilimia 85** kwa Vijijini na **asilima 95** kwa Mijini ifikapo mwaka 2025. Msisitizo wa Kamati ni Serikali kuendelea kuiwezesha Sekta hii kupata fedha kadiri inavyoidhinishiwa na Bunge.

## 3.3 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.3.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji – **Fungu 49** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naomba kubainisha Maoni ya Kamati ambayo

yamezingatia changamoto zinazoikabili Sekta ya maji. Changamoto hizo ni pamoja na: -

(a) Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi mikubwa ya Kimkakati ya maji;

(b) Baadhi ya Taasisi za Serikali kutokulipa deni la **Shilingi 61,421,854,197.67** kwa Ankara za huduma ya maji iliyotolewa na Mamlaka za maji

(c) Malimbikizo ya madeni ya Wakandarasi kiasi cha **534,725,071,524.31**

(d) Uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji;

(e) Uelewa mdogo wa Jamii juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na ongezeko la watu linalosababisha kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi;

(f) Mabadiliko ya tabianchi; na

(g) Uendelevu wa miradi ya maji katika baadhi ya maeneo ya Vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Kwa ujumla Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni mzuri ambao ni **asilimia 71.1** ya fedha zote za Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2024/2025;

(b) Utolewaji wa fedha za ndani kwa Miradi ya Maendeleo unaridhisha. Aidha, utolewaji wa fedha za nje hauridhishi.

(c) Baadhi ya Taasisi za Serikali kutokulipa kwa wakati madeni ya Ankara za matumizi ya huduma zinazotolewa na Mamlaka za maji nchini kunapunguza uwezo wa Mamlaka wa kujiendesha. Taasisi hizo na kiasi kinachodaiwa ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 8**

**JEDWALI NA. 8: Orodha ya Taasisi za Serikali zinazodaiwa na Mamlaka za Maji**

| Na | TAASISI | KIASI KINACHODAIWA |
|---|---|---|
| 1 | JWTZ | 34515091188 |
| 2 | Jeshi la Magereza | 11089534557 |
| 3 | Jeshi la Polisi | 10989275115 |
| 4 | Hospitali za Mikoa (Wizara ya Afya) | 1,688,709,627.20 |
| 5 | Mifugo na Kilimo | 225,052,719.28 |
| 6 | Ikulu Ndogo | 287,818,135.79 |
| 7 | Serikali za Mitaa | 2,442,659,137.23 |
| 8 | Maliasili na Utalii | 122,306,646.02 |
| 9 | Mahakama | 61,407,072.10 |
| | **JUMLA** | **61,421,854,197.7** |

(c) Kutokulipa madeni ya Wakandarasi kwa wakati kunakwamisha utekelezaji wa miradi ya maji na kuchelewesha Wananchi kunufaika na miradi katika maeneo hayo;

(d) Utekelezaji wa Mkakati wa kuwa na grid ya Taifa ya Maji utasaidia kupunguza uhitaji wa maji katika maeneo mengi nchini;

(e) Kutokusambazwa kwa maji katika baadhi ya Maeneo ambapo miradi ya maji imekamilika kunasababisha Wananchi kukosa majisafi na salama wakati Serikali tayari imetumia gharama nyingi;

(f) Haja ya kuwa na Mkakati endelevu wa kutumia vyanzo vya uhakika vya maji kama ilivyoanza katika Ziwa Victoria;

(g) Haja ya Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Wizara nyingine kulinda maeneo yanayozunguka Mabwawa ya Maji kwa mujibu wa Sheria ikiwa ni pamoja na kudhibiti shughuli zisizokuwa rafiki wa mazingira ili kuwezesha Wananchi kunufaika na uwepo wa Mabwawa hayo kwa muda mrefu zaidi;

(h) Umuhimu wa Wizara ya Maji kushirikiana na Wizara ya Mifugo katika Maeneo ya mabwawa kuzingatia Miundombinu ya Maji ya kunyweshea Mifugo;

(i) Upungufu wa Lita za maji **Milioni 68** kwa siku katika Jiji la Dodoma unatokana na ongezeko la watu na shughuli za maendeleo; na

(j) Kufungwa kwa Mita janja kunaweza kuwa suluhu ya ulimbikizaji wa madeni ya Ankara za maji hususani kwenye Taasisi za Umma.

### 3.3.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na Maoni yaliyobainishwa hapo juu naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:

(a) Kutokana na fedha za maendeleo kutoka nje kutolewa kwa kiwango cha chini sana, Serikali ihakikishe fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo zinatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu.

(b) Kutokana na uhitaji mkubwa wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya Kimkakati ya maji, Serikali iangalie namna ya kupata fedha kutoka vyanzo vingine ikiwemo: -

i) Fedha zitokanazo na Tozo ya **Shilingi 50** kwa kila lita ya disel na petrol kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Maji zitolewe kwa wakati na kwa ukamilifu;

ii) Kuandika maandiko ya kutafuta fedha kwa Washirika wa Maendeleo; na

iii) Kuhamasisha Mamlaka ya Maji - Tanga UWASA Bond kufanya vizuri ili Mamlaka zingine ziige;

(c) Taasisi tisa za Umma zinazodaiwa Ankara za Matumizi ya huduma za Maji kiasi cha **Shilingi 61,421,854,197.7** zilipe madeni hayo kabla ya tarehe 30 Juni 2025 ili kuziwezesha Mamlaka za Maji kujiendesha.

(d) Serikali ilipe madai ya wakandarasi kiasi cha **Shilingi 534,725,071,524.31 kabla ya tarehe 30 Juni,2025** ili kuepukana na madhara yanayoweza kujitokeza kwa kutopatikana kwa fedha hizo. Miongoni mwa madhara hayo ni:-

(i) Kuchelewa kukamilika au kukwama kwa miradi ambayo tayari imeanza kutekelezwa na kuigharimu Serikali fedha nyingi;

(ii) Kuiongezea Serikali gharama kutokana na miradi kutokamilika kwa mujibu wa Mikataba;

(iii) Kupunguza/kuondoa imani ya wananchi kwa Serikali yao;

(iv) Kuwakwamisha Wakandarasi hususani watoa huduma Wakandarasi wadogo wa ndani; na

(v) Kuchelewa /kutotekeleza azma ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani na kutekeleza ahadi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 ya kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waishio Vijijini inafikia zaidi ya **asilimia 85** na zaidi ya **asilimia 95** kwa Mijini ifikapo mwishoni mwa mwaka **2025.**

(e) Serikali iandae Mpango Kabambe wa uendelezaji wa Sekta ya Maji (National Water Master Plan) utakaohusisha kuwa na Grid ya Taifa ya Maji

(National Water Grid) kwa kutumia vyanzo vya Maziwa makubwa na Mito mikubwa ili kuimarisha utoaji wa huduma ya Majisafi na salama nchini.

(f) Serikali iweke kipaumbele kukamilisha miradi ambayo tayari imeanza kutekelezwa badala ya kuwa na miradi mingi ambayo haijakamilika. Aidha, Serikali isambaze maji katika maeneo ambapo miradi ya maji imekamilika ili Wananchi wanufaike na huduma ya majisafi na salama.

(g) Fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji zitokanazo na Tozo ya diseli na petroli zitolewe kama zilivyokusudiwa kwa wakati na kwa ukamilifu;

(h) Ili kuwa na ulinzi wa vyanzo vya maji ikiwemo Mabwawa na kuwa na matumizi sahihi ya maji Wizara ya Maji: -

i) Ishirikiane na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi ili kulinda maeneo yanayozunguka Mabwawa ya Maji kwa mujibu wa Sheria;

ii) Kudhibiti shughuli zisizokuwa rafiki kwa Mazingira ili kuwezesha wananchi kunufaika na uwepo wa mabwawa hayo kwa muda mrefu zaidi;

iii) Ishirikiane na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika maeneo ya Mabwawa kuzingatia Miundombinu ya Maji ya kunyweshea Mifugo; na

iv) Iendelee kuwashirikisha Wananchi kwenye uandaaji na utekelezaji wa miradi ya maji

(i) Ili kukabiliana na upungufu wa takribani Lita **Milioni 68** za maji kwa siku katika Jiji la Dodoma. Serikali; -

i) Iendelee na jitihada za kujenga miradi ya maji ya muda mfupi ikiwemo kuchimba Visima ili Wananchi waweze kupata huduma ya majisafi na salama, wakati wakisubiri miradi mikubwa kutekelezwa;

ii) Serikali itenge fedha za kutosha katika utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ikiwemo ya Farkwa na Ziwa Victoria ili kuharakisha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma na kunufaisha Wananchi wengi zaidi;

(j) Serikali ifunge Mita janja hususani kwenye Taasisi za Serikali ili kuepusha malimbikizo ya madeni na kudhibiti upotevu wa maji;

(k) Kwa dhamira ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi Wizara ya Maji: -

i) Ishirikiane na Wizara nyingine ikiwemo, TAMISEMI, na Wizara ya Ardhi, kuandaa Mwongozo utakaoelekeza kila mkazi anapoomba kibali cha ujenzi kuweka miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua.

ii) Iweke Mpango mahsusi wa kujenga Mabwawa mengi kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua.

### 3.3.3 Hitimisho

#### (a) Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati kwa mara nyingine napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako madhubuti. Kamati yangu inakuahidi ushirikiano wa hali ya juu na tunakuombea afya njema, Maisha marefu na ushindi katika safari ya Oktoba,2025. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia katika kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hususan wakati wa Uchambuzi wa Bajeti na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa Wajumbe wa Kamati ningetamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Jackson Gedion Kiswaga Mb | - | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Anna Richard. Lupembe, Mb | - | **M/Mwenyekiti** |
| 3. | Mhe. Asya Sharif Omar, Mb | - | **Mjumbe** |
| 4. | Mhe. Mohammed Jumah Soud, Mb | - | **Mjumbe** |
| 5. | Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb | - | **Mjumbe** |
| 6. | Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb | - | **Mjumbe** |
| 7. | Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb | - | **Mjumbe** |
| 8. | Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb | - | **Mjumbe** |
| 9. | Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb | - | **Mjumbe** |
| 10 | Mhe. Regina Ndege Qwaray, Mb | - | **Mjumbe** |
| 11 | Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb | - | **Mjumbe** |
| 12 | Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb | - | **Mjumbe** |
| 13 | Mhe. Keneth Nollo, Mb | - | **Mjumbe** |
| 14 | Mhe. Suleiman Omar Mohamed, Mb | - | **Mjumbe** |
| 15 | Mhe. Ritta Kabati Enespher, Mb | - | **Mjumbe** |
| 16 | Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Mb | - | **Mjumbe** |
| 17 | Mhe. Charles Mwijage, Mb | - | **Mjumbe** |
| 18 | Mhe. Deo Kasenyanda Sanga, Mb | - | **Mjumbe** |
| 19 | Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb | - | **Mjumbe** |
| 20 | Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb | - | **Mjumbe** |
| 21 | Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni, Mb | - | **Mjumbe** |

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji Mheshimiwa **Jumaa Aweso,** (Mb) na Naibu Waziri Mheshimiwa **Mhandisi Kundo Mathew** (Mb), Katibu Mkuu **Mhandisi Mwajuma Waziri,** Naibu Katibu Mkuu **Ndugu Agness Meena** pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano waliotupatia Kamati wakati wa kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge **Ndugu Baraka Ildephonce Leonard,** kwa umakini na weledi katika kuratibu shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama.

**(b) Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji **Fungu 49** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jackson G. Kiswaga, Mb,
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**MAJI NA MAZINGIRA.**

08 Mei, 2025.